

NAFASI ZA AJIRA

Anazak ni shule ya awali na msingi inayotoa elimu bora kwa watoto kuanzia miaka 2-12. Shule ya Anazak inapatikana eneo la Kimara temboni wilaya ya Ubungo, Kata ya Saranga, Mkoa wa Dar es salaam. Anazak ni shule ya kisasa yenye walimu mahiri inayotumia vifaa vya kisasa kuhakikisha inatoa elimu bora. Watoto wanasimamiwa na kufundishwa na kujengwa vizuri katika Nyanja za kitaaluma na kijamii.

Anazak inaamini katika ushirikishwaji na ubunifu pia kuzingatia mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi wake kwa kujali utu na heshima.

Anazak inaalika watazania wenye sifa kuomba kujaza nafasi zifuatazo:

1. Wahudumu wa bweni wa kike (nafasi 4)
2. Muokaji wa mikate wa kiume (nafasi 1)
3. Mpishi wa kiume (nafasi 1)

Eneo la kazi: Dar es salaam, Tanzania

Mshahara: Makubaliano kulingana na uwezo, ujuzi na uzoefu wa kazi

Sifa za kitaaluma ujuzi pamoja na uzoefu

- Elimu ya kidato cha nne
- Awe na uzoefu wa kazi anayoomba angalau kwa miaka isiyopungua miwili
- Awe anaweza kuwasiliana vizuri kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza
- Awe anajua kusoma na kuandika vizuri
- Awe na uwezo wa kutunza kumbukumbu mbalimbali

Masharti ya ajira kwa waombaji wote

- Muhudumu wa bweni awe tayari kukaa shuleni wakati wote kwani shule ni ya bweni
- Mhudumu wa bweni mwenye umri wa miaka 30-35 maombi yake yatazingatiwa zaidi
- Waombaji wote wanapaswa kuwa waadilifu wasiokuwa na rekodi ya uhalifu
- Waombaji wote wanapaswa kuambatanisha maelezo binafsi (cv), elimu, ujuzi na uzoefu wa kazi pamoja barua (2) za wadhamini
- Picha ya passport size ya hivi karibuni
- Kitambulisho cha taifa au namba ya Nida.

Aina ya ajira: ni ajira ya kudumu

Zingatia :

Muombaji atume maombi yake aambatanishe wasifu na vyeti vyake vya taaluma kwa anuani ya

Anazak Pre-and primary school

P.o.Box 71306

Dar es Salaam

info@anazakschools.sc.tz or

hr@anazakschools.sc.tz

Au maombi yaletwe kwa mkono shuleni Anazak

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe:11th **Disemba 2024 saa 11:00 Asubuhi**